MSHAIRI WA KISWAHILI NA LUGHA YAKE

Mvita na Pwani yote ya Kenya in wingi wa *malenga* na washairi. Bwana Nabhani ni mmoja wapo wa wataalamu ambao wamo mbioni kuikuza lugha ya Kiswahili na kuwaongoza wahitajiao maongozi katika ushairi na umalenga - MHARIRI

• AHMED SHEIKH NABHANI

NA Ahmed Sheikh Nabhani

USHAIRI ni chombo kimoja katika vyombo muhimu vya kuelezea utamaduni wa Waswahili na mshairi wa Kiswahili hukitumia chombo hiki katika bahari mbali mbali. Akipenda, aweza kutumia bahari ya shairi, wimbo, utendi (utenzi), tumbuizo, ukawafi, wajiwaji na kadhalika. Bahari hizi zategemea mpangilio wa mishororo, mizani na vina na pia maudhui ya kile atakachokusudia kukieleza.

Na mshairi wa Kiswahili anapoandika tungo zake aghalabu hapendelei kuweka wazi ayaelezayo bali hutumia njia ya **uketo**, yaani njia ya undani. Sheria za kutunga katika desturi za Kiswahili zamtaraji atumie njia ya **uketo** ili msomaji mwenyewe aweze kufahamu aelezwa nini. **Uketo** umegawanyika katika sehemu nne maarufu.

Kwanza, ni tungo za **uwazi**: mtu akielezwa jambo atafahamu aelezwa nini. Tungo nyingi katika magazeti na majarida siku hizi ni za aina hizi.

Pili, tungo za **fumbo** hutumiwa kuelezea jambo. Hapa pana ugumu mkubwa: kufungiwa **fumbo** lazima atumie bongo lake ili aweze kufahamu anaelezwa kitu gani na aweze kulifungua fumbo lile.

Tatu, ni tungo za **mfano** ambazo hutumiwa na mshairi kumwelezea mtu jambo fulani kwa kumpigia mfano kwa sababu hawezi kumweleza kwa uwazi; mtu anayeelezwa kwa njia hii atafahamu au pengine asifahamu.

Nne, tungo za **mafunzo** ya lugha hutumiwa pia na baadhi ya washairi.

Mfano mmoja wa **uketo** wa tungo za **fumbo** ni utenzi wa fumo Liyongo (1160-1204A.D.) aliyeishi Shaka karibu na Kipini huko Lamu, Kenya, na aliyejulikana kwa ushujaa wake na ubingwa wake katika tungo. Alitunga utendi - *mwana Ninga* - wa kumsifu mkewe. Alieleza baadhi ya mambo waziwazi na baadhi akayafumba kwa sababu mila na desturi za Kiswahili hazimruhusu mtu kuweka kitu wazi mbele ya hadhara ya watu; lazima afumbe ili yule tu anayaweza kufahamu kinachosemwa aelewe.

Fumo Liyongo alimsifu mkewe kutoka kichwani mpaka miguuni kwa beti 52. Alipoeleza sifa za ndani za mkewe hakuzitasua bali alizifumba.

Fumo liyongo alieleza mambo ambayo yakisomwa mbele ya hadhara ya watu hakuna atakayeona haya, lakini ni mambo ambayo, kwa kawaida, hayatasuliwi hadharani. Aliyafinika.

Lakini siku hizi inasikitisha kuona washairi wakiweka wazi yote waelezayo - kinyume kabisa na sheria za kutungu katika desturi za Kiswahili.

Mfano wa shairi la **mfano** ni wa Ali Koti - jina lake hasa lilikuwa Ali Athmani - aliyekuwa mshairi hodari sana wa mji wa Pate (1700-1800 A.D.). Alikuwa akitunga mashairi ya kumtukana mfalme wa Siu, mji jirani na Pate. Siku moja - wakati ambapo hakukuwa na vita tena baina ya miji hiyo miwili - watu kadhaa walialikwa mjini Siu; na Ali Koti, kwa kuwa alikuwa mshairi mashuhuri, pia alialkwa. Mfalme wa Siu alipopata habari kuwa Ali Koti alikuwako karamuni, alimwambia joma (askari) kuwa baada ya karamu amzuie Ali Koti asiondoke. Mfalme bado alikuwa nayo moyoni mambo Ali Koti zamani aliyokuwa akiyaandika kumtukania. Na Ali Koti naye, kwa kuwa alikuwa ni mshairi na mtu mwenye nadhari, alihisi kuwa palikuwa na jambo fulani hapo karamuni ambalo lingeweza kumletea hatari au madhara. Alipofika mlangoni baada ya karamu, joma akamwambia: "Tumeamriwa tusikuliche kuondoka," yaani wasimwache kuondoka. Pale pale akatumia neno 'licha' na kutunga ubeti huu:

Licha kuwa langishiwe, hata kama laanguka,
Ukadhihiri ufawe, pasina kuumunika,
Ukipowa sikuliwe, kwani halikupunguka,
Shahasi lingaanguka, halitwi ina lingine.

Maana yake, 'shahasi' (chombo kivaliwacho puani), hata kama likianguka na kuingia ufa, bado ni 'shahasi' vile vile - yaani, mfalme hata kama akitukanwa ni mfalme vile vile na ufalme wake haukupunguka. Mfalme akaamrisha Ali Koti aachiliwe aende zake na akamsamehe.

Mfano mwingine wa utungo unaolezea mambo kwa **mfano** ni wa mtu ambaye, baada ya kufarakana na mkewe baada ya kuishi kwa masikizano na kubarikiwa watoto, alileta majuto baadaye na akafanya bidii arudiane naye. Akamtungia wimbo akimlaumu:

Walimuinabu, ukimemetuka,
Fedha na dhahabu, zikitawanyika,
Umejiharibu, umeharibika.

Na bibi, ambaye alipoachwa na mumewe alikuwa akipata shida ya kupata chakula kwa ajili yake mwenyewe na watoto, akamjibu hivi kwa vile alijua hakuwa na makosa.

Tini na ratabu, zimbetwe na chaka,
Hazina shirabu, mayani hupuka,
Waloniharibu, ni wewe kumbuka.

Yaani, watoto wake ('tini' na 'ratabu') walikuwa na njaa ('chaka') na hukosa chakula ('shirabu'), ndiyo maana yeye akiwa katika hali hiyo; alikuwa aking'ara kwa 'fedha' na 'dhahabu' zamani na kama bwana asingemwacha 'asingeharibika' kwa kutafuta msaada kwa watu.

Mfano wa tatu wa utungo wa **mfano** ni wa mtu mmoja aliyekuwa na hamu sana kufanya urafiki na bibi mmoja kwa ajili ya kumwoa. Akamtungaia na kumpelekea utungo huu:

Naliota tangamano, ziweoni kikuweka,
Karusha wangu mkono, kakudara kashutuka,
Kaupija mto meno, matozi yakinishuka.

Yule bibi akamjibu:

Changu cha feruzi kito, kinivemeo na moyo,
Kituzo changu cha mato, kinisao wayowayo,
Lau nangalikuwa mto, kakinga matozi hayo.

Yaani, angependa kufanya 'tangamano' na huyo bwana lakini alikuwa amekwisha poswa na mtu mwengine ... angekuwa hajaposwa ... kubali kufanya 'tangamano' ... ye ('lau nangalikuwa mto, kakinga matozi hayo'). H... huyu ametumia njia ya ... ya kumkatalia ingawa ... aweza kuchukulia ... bibi alikubali kuunga ... bwana huyu kwa ... ndoa.

Mwisho, ni tungo za ... **disho** ya lugha amba... miwa kuwataka wato... ze kufungua fumbo ... msamiati vile vile. M... wa wimbo - Ngisi - u... sha msomaji tofauti ka... viwili viwili vinavyo... katika makumbo m... kama vilo ubahari... ukulima na kadhalika.

Unahudha ungadia, u... huisi,
Kupija kifuwa mai, ...
yambo rahisi,
Na Dome humtambu...
kumwita Ngisi?

Kuna Matusha na Tui, ...
ni udamisi,
Mataza ni mwende Ui, ...
kilo kipesi?
Mwenye mato halum...
da humwita Farasi.

Huyuwi huitambui, ...
Ilimasi,
Ngandu huifafanui, S...
chako kiyasi,
Simba kumwita Tui, ...
ama huisi.

Jahazi hupija dui, kula...
unasi,
Keekee haizui, imek...
gosi,
Hini ajabu nda mui, ...
kumcha fisi.

Chalozama hukizui, hat...
karatasi,
Chalopwewa hukish...
nguvu na zako kasi,
Mwenye mato haone...
henda hapapasi.

Basi siku zote uketo ... go ni wa aina mbali... washairi wa zamani ... wakitunga hivi. Na sisi ... tufuate hatua na ... kwa kutungu kama wao.

Coastweek * JEMBE**

SWAHILI CROSSWORD NO. 3

Washindi wa Fumbo La Kujaza Maneno No. 1:
(1) Juma Mwayani wa P.O. Box 96128, Likoni, Mombasa,
na
(2) Mohammed Abdalla wa P.O. Box 98702, Mombasa.
Washindi waombwa wafike Afisini mwa COASTWEEK.

KWENDA KULIA:

1. Umoja wa Matifa
4. Huvuliwa kwenye chanda
8. Yakutafunia
120. Fahali
12. Neno "Kanju" imepungua herufi moja
13. Kusema, Kusengenya
14. East African Marketing Board
16. Aer kama ilivyo
18. Atoa roho
20. Mila, desturi
23. Kinyume cha anika
26. Si hawa
28. Samli kwa Kimombo
30. Kulinda shamba
31. Bora
32. Mmea wa dawa
33. Herufi IEI

KWENDA CHINI:

1. Shika kwa meno
2. Kinyume cha nyembamba
3. Jaribu utamu
5. Matanga ya mke kufiwa na mumewe
6. Peleka mtu mahali fulani
7. Aina ya tunda
9. Jina la Kijaluo
11. Wingi wa sikio kwa Kimombo
15. Mti wa mtama
17. Sehemu ya ndege
19. Hewa
21. Hutembea katika mishipa
22. Atoa machozi
24. Maisha
25. Aele kama ilivyo
27. Kula kwa Kimombo
29. Herufi EII

Shindano la fumbo la kujaza maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindi wawili wa kwanza kila mmoja atapatiwa bandali moja la Unga Wa Mahindi chapa Jembe.

Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK LTD., pamoja na ATTA LTD., Mombasa.

Jawabu za fumbo hili, lipelekwe kwa muhariri COASTWEEK, sanduku la posta 87270, Mombasa, Kenya, siku ya Alhamisi tarehe 30.11.78, saa sita mchana shindano hili litakuwa mwisho.

JEMBE
UNGA SAFI NO.1
WA MAHINDI

KWA UFUPI

MWENYEKITI wa Kanu huko Voi, Bwana Raphael Mzee Mwazala naye alisaidia kuchangisha zaidi ya shillingi elfu nne kwa kusaidia kanisa la Mkwachunyi CPK Church huko Mbololo.

***

HUKO Hola, Polisi wanawasaaka majimbazi ambao huingia katika nyumba wakati wa usiku wakiiba vyakula na kutoweka.

MKUU wa mpango wa kutia mataa katika kiwnaja cha michezo cha manispaa ya Mombasa Bwana C. Ondato amedokeza kwamba kamati yake imekusanya zaidi ya shillingi 200,000 kwa mpango huo utakaogharimu zaidi ya shillingi 1.3 millioni kuukamilisha. Alitoa mwito kwa wananchi kuunga mkono mpango huo na misaada kutoka kwa Makampuni. Alisema wizara ya Huduma za jamii na nyumba nchini Kenya imetoa shillingi 100,000 kuusaidia mpango huo.

BANKI ya shirika nchini ... itaimarisha utumishi wa... kuanzisha idara mpya ... dumia wanachama. Aki... haya Mwenyekiti wa B... Shirika nchini Kenya, ... Bernard Kathanga alisema ... kubuniwa kwa Banki hiyo ... la ya shillingi 600,000,000 ... shatolewa kama mikopo ... vyasikirika. Bwana K... alikuwa akitembelea W... eneza Sanaa wa Akamba H... icraft Mjini Mombasa.

***

COFFY KATIKU
na Jimmy Mazoweya, Mombasa High School

Bi-Coffy Katiku ni mzalia wa Pwani ya Kenya, mtaalamu wa kazi za afisini, na msimamizi wa taratibu za shule ya Mombasa High School.

Ana moyo wa utumishi, juhudi na uaminifu.

Bi-katiku husimamia mipango yote ya shule akiwa katibu wa mkuu wa shule, na kutumikia walimu, na wanafunzi kwa utaratibu na ufanasi.

Hupenda kuogelea, kupanda Honda, kuendesha gari na kusoma magazeti.